

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU**

## **MASHARTI YA KUPATA LESENI YA BIASHARA**

- Mtu yejote rai wa Tanzania anayo haki ya kupatiwa leseni ya biashara ili mradi awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane (18) mwenye akili timamu ambaye hajawahi kupatikana na kosa la jinai, awe na eneo la kufanya biashara linalokubalika kisheria.
- Kwa mtu ambaye sio raia wa Tanzania anapaswa kuwa na kibali kinachomruhusu kufanya biashara nchini kutoka Idara ya Uhamiaji.

## **UTARATIBU WA KUPATA LESENI YA BIASHARA**

- i. Mwombaji anapaswa kujaza fomu ya maombi 9TFN 2110 kikamilifu na kuambatanisha kivuli cha: - Jina la Biashara kama sio mtu binafsi (Certificate of Incorporation or Registration).
- ii. "Memorandum and Article of Association" kama ni Kampuni.
- iii. Kitambulisho cha mpigakura, Cheti cha kuzaliwa au Hati ya kiapo kuonyesha kuwa ni Mtanzania na Mgeni Hati ya kuishi Nchini daraja la "A" (Residence Permit Class "A").
- iv. Hati ya kiuwakili (prowess of a Honey) kama wenyewe hisa wote wa Kampuni wapo nje ya nchi.
- v. Ushahidi wa maandishi kuwa ana mahali pa kufanya biashara (Kwa mfano hati za nyumba, mkataba wa upangishaji, risiti za malipo ya kodi za majengo au ardhi).
- vi. Hati ya kujiandikisha kama mlipa kodi TRA (TIN).
- vii. Kuwa na hati ya kutodaiwa kodi ya TRA (Tax Clearance Certificate).

Kwa leseni zinazodhibitiwa na Mamlaka mbalimbali, Kwa mfano (TFDA, EWURA, TAURA, CRB, TILLI) n.k lazima mwombaji kuwa na leseni husika kabla ya kuomba leseni ya biashara fomu ya maombi ya biashara (TFN 211) hutolewa kwa ada ya Tshs. 2,000/=. Baada ya kujaza fomu na viambatanisho, maombi hupitishwa ngazi zinazotakiwa kisheria – Mpango Miji na Afya. Baada ya hapo leseni hutolewa ndani ya siku moja au mbili na si zaidi. 2

**Angalizo:** Kwa utaratibu wa kuanzia mwaka 2013/2014 leseni zote hutolewa kwa malipo ya ada za leseni na leseni zote hutolewa kwa kila Mwaka kwa mujibu wa sheria ya leseni ya Biashara Na. 25 ya mwaka 1972 na mabadiliko yake.

### **MASHARTI YA UTUMIAJI WA LESENI**

- i. Mwenye leseni hataweka masharti yejote kwa mnunuzi.
- ii. Mwenye leseni atatoa risiti kwa mauzo yote.
- iii. Mwenye leseni atafuata sheria ya leseni ya Biashara Na. 25 ya 1972.
- iv. Mwenye leseni hatapewa huduma/bidhaaa ambazo hazizingatii viwango vya ubora uliowekwa na vyombo vinavyotumika kisheria.
- v. Mwenye leseni anaweza kunyan'ganya wakati wowote ikiwa itaonekana aliiapata kwa njia ya danganyifu au amekiuka masharti ya leseni.

### **MAKOSA**

- i. Kuendesha biashara bila leseni.
- ii. Kuendesha biashara eneo tofauti na linaloonyeshwa kwenye leseni.
- iii. Kutumia leseni moja kufanya biashara zaidi ya moja au maeneo mawili au zaidi.
- iv. Kushindwa kuonyesha leseni ya biashara inapotakiwa kufanya hivyo na Afisa aliyeidhinishwa na Serikali.
- v. Kutokuweka leseni ya biashara mahali ambapo inaonekana kwa urahisi.
- vi. Kutoa maelezo ya uongo ili kupata leseni au kukwepa kulipa ada/kodi inayostahili.
- vii. Kumzuia Afisa wa Serikali aliyepewa mamlaka ya kukagua au kufanya kazi yake.

### **3. ADHABU**

Mtu yeote anayetenda mojawapo ya makosa hapo juu adhabu yake ni faini isiyopungua Tshs.50,000/= na isiyozidi Tshs. 100,000/= au kifungo kisichozidi miaka miwili (2) au faini na kifungo kwa pamoja.

### **UTAWALA**